maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari............... Bado kitambo kidogo nanyi hamnioni; na tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona.” (Yohana 16:12-16).

Huyu ndiye Muhammad s.a.w. aliyeleta kweli yote kwa njia ya ufunuo alioupokea toka kwa Mungu wenye sura zenye kuanza kwa jina la Mungu, ***Bismillah,*** kama vile Yesu alivyobashiri sehemu nyingine pale aliposema: Hamtaniona kamwe tangu sasa hata mtakaposema amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana (Mathayo 23:39). Ili wafuasi wake waweze kumuona tena, itabidi kwanza wamkubali na kumsema kuwa ni mtu aliyebarikiwa yule nabii atakayekuja na mafundisho yaliyo ufunuo mtupu wa Bwana (Mungu), yaani Muhammad s.a.w. na ndivyo walivyofanya wale ndugu zetu wapenzi wakristo walipomuona Mtume s.a.w. na ambao Mungu Amewasifu sana katika aya iliyodhihirishwa hapo juu. Kwani ujio wa Isa wa mara ya pili utaambatana na nabii huyo aitwaye roho wa kweli, akitokea ndani ya umati wa huyo roho wa kweli, kwa njia ya mfano, kwa dhati ya nabii mwingine, kama vile alivyodhihiri Eliya mara ya pili kwa njia ya mfano kwa dhati ya nabii mwingine aliyeitwa Yohana Mbatizaji (Mathayo 11:13-14).

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ndiye aliyedhihiri katika zama zetu hizi na kuutangazia ulimwengu kuwa yeye ndiye yule Isa bin Mariam anayesubiriwa na Wakristo kwa Waislamu kuja kuwaongoza wanadamu wote kwenye njia sahihi iliyopitwa na manabii wote pamoja na wafuasi wao, akiwa ametokea ndani ya dini ya Islam, dini ambayo imejumuisha mafundisho yote muhimu yaliyofundishwa kwa manabii wote waliopita na hivyo kuwa na uwezo wa kuwaunganisha watu wa kila dini katika dini moja. Karibuni ndugu zetu wapendwa tuungane pamoja na kueneza amani na upendo duniani chini ya himaya ya Yesu aliyekwisha dhihiri duniani kwa dhati ya nabii Mirza Ghulam Ahmad aliyetokea upande wa Mashariki huko Punjab India katika kijiji cha Qadian.

TOVUTI YETU: www.alislam.org.

**Taarifa za kituo chetu cha**

**MUSLIM TELEVISION AHMADIYYA (MTA)**

ambacho kinafanya kazi muda wote ni:-

**MTA FREQUENCY-12015.V**
**SYMBOL RATE - 29,950**
**SAT SES.5**

**Anuani :-**

Ukiwa na maswali zaidi unaweza kuwasiliana na wabashiri wetu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya nchini kote, kwa:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Arusha/Kilimanjaro | 0787 770 655 |
| 2. | Dar es Salaam | 0655 105 096 |
| 3. | Dar es Salaam | 0620 124 768 |
| 4. | Dodoma/Singida | 0782 919 298 |
| 5. | Iringa | 0715 884 800 |
| 6. | Kagera | 0716 682 063 |
| 7. | Kigoma | 0716 045 918 |
| 8. | Mara | 0785 676 614 |
| 9. | Mbeya | 0714 266 800 |
| 10. | Morogoro | 0714 601 191 |
| 11. | Mtwara / Lindi | 0656 116 652 |
| 12. | Mwanza | 0788 677 509 |
| 13. | Pwani | 0623 228 033 |
| 14. | Shinyanga | 0788 676 618 |
| 15. | Songea | 0656 116 698 |
| 16. | Tabora | 0788 677 433 |
| 17. | Tanga | 0714 583 380 |
| 18. | Tunduru | 0655 028 203 |
| 19. | Zanzibar | 0675 321 543 |

لَآ إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

**Hapana Apasaye kuabudiwa ila Allah**
**Muhammad ni Mtume wa Allah**

# UISLAM HAUNA UADUI NA UKRISTO

**Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
**P.O. Box 376, Dar es Salaam.**
**Mnazimmoja, barabara ya Bibi Titi.**
**Mkabala na Bustani ndogo ya Mnazimmoja**
**Email: ahmusjamtaz@gmail.com**

**Imechapishwa na:**
**Ahmadiyya Printing Press Tanzania**
**Mob: 0715 771 813**
**Email: ahmadiyyaprintingpresstz@gmail.com**

بســـــم‌الله‌الـرَّحـمــن‌الـرَّحـــيــــــــم

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu***

# UISLAM HAUNA UADUI NA UKRISTO

Ndugu zetu Wakristo wanajinasibisha na Nabii mtakatifu sana wa Mwenyezi Mungu, Nabii Isa a.s., aliyetokana na uzao wa Nabii Ibrahim a.s. na sisi Waislamu twajinasibisha na mbora wa mitume wote, Mtume Muhammad s.a.w. ambaye naye pia alitokana na uzao wa Nabii Ibrahim a.s. Kurani Tukufu imewataja ndugu zetu hao Wakristo kwa heshima na taadhima na kuwaita kwa jina la Naswaaraa, yaani wale waliomsaidia Nabii Isa a.s. katika kazi yake aliyokabidhiwa na Mwenyezi Mungu. Kurani Tukufu inasema: Na kumbukeni Isa bin Mariam alipowaambia wafuasi wake; ni nani walio wasaidizi wangu katika njia ya Allah. Wakasema wafuasi wake sisi ni wasaidizi wa Allah. Basi kundi moja miongoni mwa wana wa Israeli likaamini na kundi lingine likakufuru. Basi tukawasaidia wale walioamini dhidi ya maadui zao nao wakawa ndio washindi. (61:15). Hawa walioamini ndio ambao siku hizi wanajulikana kama Wakristo na ndio sababu tunalazimika kuwapenda na kuwahurumia kwa moyo mkunjufu, kwani walimsaidia nabii wa Mwenyezi Mungu, Isa bin Mariam, ambaye tunampenda sana na kumuheshimu sana.

Sehemu nyingine ndani ya Sura 18:14-16 Mwenyezi Mungu Anawaenzi ndugu zetu Wakristo kwa kusema: “Sisi Tunakusimulia habari zao kwa haki: Hakika wao ni vijana waliomwamini Mola wao, nasi Tukawazidisha katika mwongozo. Na Tukaiimarisha mioyo yao, waliposimama na wakasema: Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi, hatutamwita kabisa mungu mwingine badala yake; (hapo) bila shaka tutakuwa tumesema uovu uliopitiliza. Hawa watu wetu wameshika waungu (wengine) badala Yake. Kwa nini hawaleti juu yao dalili bayana? Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye Mwenyezi Mungu uongo?”

Huu ni msimamo walioupata ndani ya vitabu vyao vitakatifu vilivyowateremkia manabii wao. Bila shaka walikuwa wamekisoma kifungu hiki kilichomo ndani ya Kumbukumbu la Torati 6:4 kisemacho: “Sikiza Ee Israeli; BWANA Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja.” Tena ndani ya Isaya 44:6 kuna andiko hili: “BWANA wa majeshi Asema hivi: Mimi ni wa kwanza na Mimi ni wa mwisho, zaidi yangu Mimi hapana Mungu...” Halikadhalika twalikuta agizo hili ndani ya kitabu cha Wafalme: “Wewe naam, wewe - peke yako ndiye Mungu wa Falme zote za dunia; wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi (2 Wafalme 19:15). Na Yesu pia akatilia mkazo zaidi pale aliposema: “Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo Uliyemtuma.” (Yohana 17:3).

Maagizo ya aina hiyo hiyo yanapatikana pia ndani ya Kitabu chetu kitukufu cha Kurani ndani ya Sura ya Al Hadid yasemayo: “Kinamtukuza Allah kila kilichomo mbinguni na ardhini, na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake. Huhuisha na Hufisha na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Yeye Ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho Naye ni wa Dhahiri na wa Siri na Yu Mjuzi wa kila kitu. Yeye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita; kisha Akastawi katika enzi........(57:3-5).

Kurani Tukufu pia imewasema kuwa wao wapo karibu zaidi na Waislamu na sio watu wenye kutakabari na sababu yake ni kwamba wanao viongozi wao wa kiroho kwa dhati ya Makasisi na watawa. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu: “Na utawaona walio karibu zaidi kwa urafiki na waaminio ni wale wanaosema kuwa sisi ni Wanaswaaraa (Wakristo). Hayo ni kwa sababu wako miongoni mwao makasisi na maruhbani, na kwa sababu wao hawatakabari (hawajivuni). (5:83).

Mbele Mwenyezi Mungu Anaendelea kuwamwagia sifa ndugu zetu hao Wakristo kwa kusema: “Na wanapoyasikia yaliyoteremshwa kwa Mtume, utaona macho yao yakichuruzika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua; wanasema: Mola wetu, tumeamini, basi utuandike pamoja na washuhudiao. Na kwa nini tusimwamini Mwenyezi Mungu na haki iliyotufikia, na tunatumai ya kwamba Mola wetu Atuingize pamoja na watu wema. Basi Mwenyezi Mungu Akawalipa, kwa yale waliyoyasema, Bustani zipitazo kati yao mito, humo watakaa. Na hayo ndio malipo ya wafanyao wema (5:84-86).

Ni nini kilichowasaidia kuiona haki kwa Mtume s.a.w. hadi wakatokwa na machozi? Ni yale maandiko yao matakatifu yaliyowasaidia kuiona nuru ya kimbingu iliyokuwa ikimeremeta kwa Mtume s.a.w. Ndani ya Kumbukumbu la Torati 18:18 Musa a.s. alishawapasha habari aliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu kwamba miongoni mwa ndugu za wana wa Waisraeli, yaani wana wa Ismaeli, Mungu Atamuinua Nabii atakayefanana na Musa a.s. ambaye yote atakayoyatamka yatakuwa ni ufunuo toka kwa Mwenyezi Mungu, na ni Muhammad s.a.w. ndiye aliyetokana na uzao wa Ismaeli aliyekuwa mwana wa Ibrahim a.s. Na huyo huyo ndiye aliyetabiriwa na Yesu kuwa atakuja na kuwaandaa wafuasi wake kumtambua na kumkubali pale aliposema: “Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahamili hivi sasa, lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa